**HALMASHAURI YA WILAYA YA BABATI**
**KIZIDUO**
**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 21/10/2021**

**WALIOHUDHURIA (WAJUMBE WA KAMATI)**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. John S. Noya | - Mwenyekiti wa H/W | - M/kiti |
| 2. | Anna P. Mbogo | - Mkurugenzi Mtendaji (W) | - Katibu |
| 3. | Mh. Yahaya H. Loya | - Makamu Mwenyekiti H/W | - Mjumbe |
| 4. | Mh. Adamu H. Ipingika | - Diwani | - Mjumbe |
| 5. | Mh. Eluthery J. Burra | - Diwani | - Mjumbe |
| 6. | Mh. Bernad G. Bajuta | - Diwani | - Mjumbe |
| 7. | Mh. Mariam A. Kwimba | - Diwani | - Mjumbe |
| 8. | Mh. Michael N. Hillbayuded | - Diwani | - Mjumbe |
| 9. | Mh. Paulo M. Maqariye | - Diwani | - Mjumbe |
| 10. | Mh. Samson S. Hilbajojo | - Diwani | - Mjumbe |
| 11. | Mh. Lucy M. Dughang | - Diwani | - Mjumbe |
| 12. | Mh. Steven S. Mollel | - Diwani | - Mjumbe |
| 13. | Mh. Zainabu O. Dodo | - Diwani | - Mjumbe |
| 14. | Mh. Keremu B. Keremu | - Diwani | - Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA (WAJUMBE WA KAMATI)**

Mh. Daniel B. Sillo - Mbunge wa Jimbo la Babati (V) - kwa taarifa

**WALIOHUDHURIA (WATAALAM)**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Halfan A. Matipula | - Katibu Tawala Wilaya ya Babati |
| 2. | Benedict S. Ntabagi | - Afisa Utumishi na Utawala (W) |
| 3. | Florida D. Kimambo | - Afisa Sheria (W) |
| 4. | Anastacy R. Bongwa | - Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 5. | Stedvant Kileo | - Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 6. | Gilbert Mbesere | - Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 7. | Isaely Makere | - Afisa Ugavi (W) |
| 8. | Getrude Kavishe | - Afisa Elimu Msingi (W) |
| 9. | David James | - Afisa Uchaguzi (W) |
| 10. | Alice G. Mwallo | - Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 11. | Deus Mbalamwezi | - Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 12. | Regina Mlinga | - Mratibu wa TASAF (W) |
| 13. | Suten Mwabulambo | - Kaimu Mganga Mkuu (W) |
| 14. | Florine Humuri | - Kaimu Afisa TEHAMA (W) |
| 15. | Alex G. Basubizahe | - Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 16. | Joseph Kuida | - Katibu TSC (W) |
| 17. | Bombo B. Gidang'ay | - Kaimu Mhandisi Ujenzi (W) |
| 18. | Leonard S. Masesa | - Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W) |
| 19. | Peter Nada | - Afisa Vifaa na Takwimu (W) |



Scanned with CamScanner

| | | | |
|---|---|---|---|
| 20. | Noel Mosha | - | Kaimu Afisa Ufugaji Nyuki (W) |
| 21. | Fabian M. Mandas | - | Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W) |
| 22. | Glane Kauleni | - | Kaimu Afisa Biashara (W) |
| 23. | Canute Francis | - | Mhasibu wa Mapato (W) |
| 24. | Miontini L. Gwandu | - | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 25. | Meshack Mhagama | - | Kaimu Afisa Usafiri (W) |
| 26. | Glory N. Absalum | - | Afisa Tarafa Bashnet |
| 27. | Msalla H. Msalla | - | Afisa Tarafa Babati- |
| 28. | Frank P. Salala | - | Kaimu Afisa Tarafa Mbugwe |
| 29. | Nada Hussein | - | Kaimu Afisa Tarafa Gorowa |

**SEKRETARIET**

1. Edith Mauki
2. Stephen Emanuel

**MUHT.NA.144/2021 – KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao baada ya akidi kutimia. Alisema kikao hicho kiliitishwa maalum kwa ajili ya kuomba kibali cha matumizi ya fedha za mkakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19.

Mwenyekiti alifungua kikao saa 3:45 asubuhi. Katika hotuba yake ya ufunguzi alisema kikao hicho kiliitishwa maalum kwa ajili ya kupitisha fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo Halmashauri ilipangiwa.

**MUHT.NA.145/2021 – KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe walithibitisha agenda zifuatazo ili zijadiliwe katika kikao hicho:-

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Taarifa ya fedha za mkakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO – 19
4. Kufunga kikao.

**MUHT.NA.146/2021 – TAARIFA YA FEDHA ZA MKAKATI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO – 19**

Katibu alieleza kuwa Halmashauri ya wilaya ya Babati ilitegemea kupokea kiasi cha shilingi **1,950,000,000.00** ikiwa ni Fedha za utekelezaji Mpango wa maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19. Fedha hizi zipo nje ya Bajeti na zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa na bweni sekta ya Elimu na ujenzi wa nyumba za watumishi sekta ya Afya. Fedha hizo zilielekezwa kutumika kwenye sekta zifuatazo:-

- **Sekta ya Elimu Sekondari**



Scanned with CamScanner

Halmashauri ilitengewa kiasi cha shilingi **1,560,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **78** ambapo kila darasa litagharimu kiasi cha shilingi 20,000,000.00.

- **Sekta ya Elimu Msingi**

Halmashauri ilitengewa kiasi cha shilingi **220,000,000.00** kwa ajili ya kujenga madarasa **11** kwenye shule shikizi 3 za Kazaroho (6), Maleshi (3) na Datari (2), pia ilitengewa kiasi cha shilingi **80,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa **Bweni 1** shule ya msingi yenye mahitaji maalum ya Dareda Kati.

- **Sekta ya Afya**

Halmashauri ilitengewa kiasi cha shilingi **90,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 1 ya watumishi (three in one) katika Hospitali ya Halmashauri – Mwada, gari la kisasa la usimamizi wa huduma za Afya na gari moja la kubeba wagonjwa (Ambulance).

Vile vile kulingana na maelekezo ya Wizara ujenzi wa madarasa ulitakiwa ukamilike kabla au ifikapo tarehe 15/12/2021 na miradi mingine ilitakiwa ikamilike tarehe 30/04/2022. Fedha hizi zilitolewa kwa ajili ya ujenzi na si ukamilishaji wa maboma. Aidha wananchi wahamasishwa kushiriki ujenzi kwa kuchimba misingi na kukusanya vifaa vinavyopatikana kwenye eneo la utekelezaji wa mradi mfano mchanga, mawe na kokoto .

Mchanganuo wa Fedha hizi, mgao kwa shule na mpango kazi wa utekelezaji wa shughuli za ujenzi uliwasilishwa kwenye kikao.

- **Mapokezi ya fedha za EP4R kwa shule za msingi Diffir Tshs. 11,872,379.86, shule ya msingi Gidewari Tshs. 11,872,379.86 na Shule ya sekondari Gidas Tshs. 11,872,379.86.**

Halmashauri kupitia akaunti za shule za Msingi Gidewari, Diffir na shule ya sekondari Gidas ilipokea kiasi cha Tshs. **35,617,139.58** ajili ya kujenga mfumo wa kunawia mikono, uvunaji wa maji ya mvua, uunganishwaji wa maji ya bomba na uchimbaji wa visima virefu.

Taarifa hii imewasilishwa kwenye kikao ili wajumbe wajadili na kutoa kibali cha kuombea vifungu kwenye Bajeti ya mwaka 2021/2022 ili fedha hizo ziweze kutumika kwa ajili ya kazi zilizopangwa.

- **Mapokezi ya fedha TSHS. 160,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya maabara katika shule ya sekondari Maganjwa na choo matundu 24 katika shule ya sekondari Dareda.**

Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilipokea fedha jumla ya Tshs. **160,000,000.00** kutoka kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

i. Ujenzi wa vyumba viwili (2) vya maabara katika shule ya sekondari Maganjwa Tshs. **120,000,000/=**
ii. Ujenzi wa choo matundu 24 katika shule ya sekondari Dareda Tshs.**40,000,000/=**



Scanned with CamScanner

Wajumbe walipokea taarifa na baada ya majadiliano walishauri:-

**Ushauri**

- Halmashauri ihakikishe miradi hiyo inasimamiwa kwa karibu na kukamilika kwa ubora na kwa muda uliopangwa.
- Timu iliyoundwa kufuatia miradi hiyo ihakikishe inakagua miradi hiyo mara kwa mara na kutatua changamoto zitakazojitokeza kwa wakati.
- Uongozi wa Kata uhakikishe timu za kusimamia miradi hiyo zinaundwa mara moja.
- Matangazo ya kuwapata mafundi wa ujenzi na vifaa yatolewe mapema.
- Makadirio ya ujenzi (BOQ) kwa ajili ya miradi hiyo yasambazwe kwenye shule zote zilizopata fedha hizo.
- Uongozi wa Kata uhamasishe wananchi kuchangia miradi hiyo.
- Uongozi wa Kata uhakikishe madawati yanaanza kutengenezwa mapema hata kabla ya ujenzi kuanza.

Baada ya majadiliano na ushauri kutolewa wajumbe waliridhia taarifa hii pamoja na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo.

**MUHT.NA.147/2021 – KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 5:55 asubuhi kwa kumshukuru Mheshimia Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipata Halmashauri fedha hizo kwani zitasaidia kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari.

Alisisitiza Waheshimiwa Madiwani na Wataalam kusimamia kwa karibu miradi hiyo ili ikamilike kwa muda uliopangwa na Serikali Kuu.

**Umethibitishwa Na:-**

| | |
|---|---|
| ................................ | ................................ |
| (Anna P. Mbogo) | (Mh. John S. Noya) |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |

**Tarehe:** 17/11/2021



Scanned with CamScanner